

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

Anwani ya Simu: "ELIMU" Simu:
026 296 35 33
Baruapepe: info@moe.go.tz
Tovuti: www.moe.go.tz



Mji wa Serikali - Mtumba,
Mtaa wa Afya,
S.L.P 10,
40479 DODOMA

Unapojibu tafadhali taja:

Kumb. Na. GA.113/277/01/34

26 Mei, 2022

Mwenyekiti,
TAMONGSCO,
S.L.P. 2662,
DODOMA

Katibu Mtendaji,
Christian Social Services Commission (CSSC),
S.L.P. 1454,
DAR ES SAALAM

Katibu Mtendaji,
Baraza la Waislam Tanzania (BAKWATA),
S.L.P. 21422,
DAR ES SAALAM

Mwenyekiti,
Tanzania Association of Private Inventors in Education (TAPIE),
S.L.P. 13346,
DAR ES SAALAM

Mwenyekiti
Baraza la Sunnah Tanzania (BASUTA),
S.L.P. 8581,
DAR ES SAALAM

Mkurugenzi,
Mtandao wa Elimu Tanzania (TEN/MET),
S.L.P. 13547,
DAR ES SALAAM.

WARAKA WA ELIMU NA. 3 WA MWAKA 2022

SARE ZA WANAFUNZI SHULENI

Tafadhali rejea kichwa cha habari hapo juu.

2. Sare ya shule ni vazi linalovaliwa na wanafunzi wa rika tofauti katika ngazi mbalimbali za elimu kuanzia elimu ya Awali, Msingi na Sekondari. Umuhimu wa uvaaji wa sare kwa wanafunzi wawapo shuleni, nje ya shule kwa ruhusa maalumu au safarini ni pamoja na:

- i. Kumtambulisha mwanafunzi mahali popote alipo ili apewe huduma stahiki;
- ii. Kufanya wanafunzi wawe na muonekano sawa bila kujali hali ya kipato cha familia ya mwanafunzi;
- iii. Kufanya wanafunzi wote waonekane nadhifu wakati wote wanapovaa sare ya shule;
- iv. Kulinda maadili ya wanafunzi kwa kuvaa nguo zenye mtindo wa ushonaji unaofanana na kukubalika kimaadili; na
- v. Kuwapunguzia wazazi mzigo wa gharama za kununua mavazi ya bei ghali ambayo yanaleta ushindani usio na tija kwa wanafunzi.

3. Historia ya sare ya shule katika nchi yetu inaonesha kwamba wanafunzi wote wamekuwa wakivaa sare ya shule wanapokuwa shuleni ama wanapotoka nje ya mipaka ya shule kwa ruhusa maalumu na wawapo safarini. Sare hii imekuwa ikishonwa na wazazi baada ya kupokea maelekezo ya aina ya sare na muonekano wake au baada ya wazazi kulipa shuleni gharama ya sare hiyo na shule kushona sare husika.

4. Kwa muda mrefu sasa, sare katika shule za Serikali zimekuwa ni shati au blauzi nyeupe na rangi yoyote ya sketi au suruali/kaptula. Hali hii imezua malalamiko miongoni mwa wadau mbalimbali wa elimu wakiwemo wazazi/walezi, waheshimiwa wabunge, wanaharakati na wanafunzi wenyewe wakidai uvaaji wa sare uzingatie mazingira ya shule ikiwemo hali ya hewa na udongo. Moja ya changamoto za uvaaji wa shati au blauzi nyeupe mahali ambapo aina ya udongo ni mwekundu ni kuchafuka kwa urahisi sana na kusababisha gharama za kufua mara kwa mara. Hali hiyo huleta changamoto kwa wanafunzi wanaotoka katika familia zenye kipato cha chini. Wakati mwingine hupelekea mwanafunzi kuadhibiwa kuwa ni mchafu kumbe mazingira alipo husababisha hali ya uchafu katika sare yake.

